

Kusanya na Ujifunze

Kata, kunja katikati, na uhifadhi



YOSHUA

KADI YA BIBLIA

1



MASWALI

- A.** Yoshua na jeshi lake waliangusha kuta za Yeriko kwa njia gani?
- B.** Kamilisha sentensi hii ya Yoshua: "Mimi na nyumba yangu, . . ."
- C.** Yoshua alijulikana kwa majina gani mengine?

4026 K.W.K.

Adamu aumbwa

98 W.K.

1 W.K.

Aliishi miaka ya 1500 K.W.K.

Kitabu cha mwisho cha Biblia kinaandikwa



YOSHUA

MAMBO MACHACHE KUMHUSU Mwana wa Nuni. Alikuwa mtumishi wa Musa na baadaye akawekwa rasmi kuongoza Israeli. (Kutoka 33:11; Kumbukumbu la Torati 34:9; Yoshua 1:1, 2) Yoshua aliwaongoza watu wa Mungu bila woga waingie katika Nchi ya Ahadi. Alitumaini ahadi za Yehova, akatii mwongozo wake, na kumtumikia kwa uaminifu.

MAJIBU

- A.** Walimtii Mungu kwa kuzunguka jiji hilo. —Yoshua 6:1-27.
- B.** ". . . tutamtumikia Yehova." —Yoshua 24:15.
- C.** Hoshea na Yehoshua. —Hesabu 13:8, 16.